

COMPANY HIGHLIGHT

# Mafunzo Majira ya Msimu wa Joto

na Geofrey Kessy

## Shule ya majira ya joto ya CMO

CMO ya Afrika ya Kusini inaandaa kozi ya uhandisi ya kila mwaka ya uhandisi kwa wataalamu wa vijana ili kuwaonyeshe vipengele tofauti vya uhandisi wa misitu. KVTC imeniwezesha kuhudhuria kozi ambayo ilikuwa fursa ya kusisimua

Sehemu ya kozi ilikuwa George katika mji wa W-Cape ya Afrika Kusini. Sehemu ya kozi ilikuwa mafunzo ya simulation ya mashine, lakini wingi ulifanyika kwenye shamba katika makampuni mbalimbali ya misitu (MTO na PG Bison), wazalishaji wa vifaa (Husqvarna, Bell, Mercedes Benz) na makandarasi ya misitu.

## Moduli ya kozi

Zifuatazo ni baadhi ya mada muhimu katika kozi hiyo

1. Mipangilio ya shughuli za mavuno na kusimamia hatari kubwa ambazo zinaathiri Usalama, Uzalishaji, Mazingira, Ubora na Jamii, mipango ya kimkakati, mbinu, ya kila mwaka na ya makundi.
2. Uchaguzi wa mifumo ya kuvuna wakati wa kutolewa kwa kutumia vigezo na gharama za usalama, uzalishaji, mazingira, ubora na jamii.
3. Gharama za mifumo ya kuvuna, mashine na tathmini ya uzalishaji.
4. Uchaguzi wa vifaa vya kuvuna na mashine, usafiri wa mbao na vifaa, matengenezo na huduma.
5. Matengenezo ya barabara za misitu, athari za kifedha na za mazingira kwenye usimamizi wa barabara za misitu.

## Fikiria

Uzoefu huo umebadilisha mbinu yangu ya kazi ya kila siku na nimepata mfiduo juu ya vipengele vya uhandisi wa misitu, kuvuna, usimamizi wa barabara za misitu na athari za kifedha kwa kila mmoja.

Tofauti na masomo hayo nilibahatika kufanya mambo tofauti kama maeneo ya utalii karibu na George na Knysna, maduka makubwa, fukwe na hata kutembelea mti wa zamani na mkubwa katika nchi ya Afrika kusini wenye umri wa miaka kadiri 800 aina ya Podocarpus falcatus huko Outeniqua.

## Umevutiwa?

Kwa habari zaidi kuhusu Shule ya Majira ya joto ya CMO, wasiliana na Andrew McEwan: andrew@cmogroup.net

HIGHLIGHTS

Neema | CRAFTS

## Neema Crafts Centre

Tunapenda kuelezea kazi nzuri inayofanywa na mteja na mbia wetu mmoja Iringa, Tanzania.

Kituo cha Uchongaji Vinyago Neema kilianzishwa 2003 na Dayosisi ya Ruaha, kutoa mafunzo na fursa ya kwa watu wenye ulemavu mkoa wa Iringa, Tanzania.

Wasanii wa Neema's wanatengeneza vinyago vya mbao, taa na thamani kutokana na mitiki ya KVTC. Wasiliana nao kwa kupitia duka la mtandao here au angalia karakana yao na bidhaa kupitia instagram handle @neemacrafts



## OSP Semina

Katika jarida la mwisho tulitangaza semina inayokuja ya OSP. Hii ilifanyika kama ilivyopangwa na karibu wakulima 450 walihudhuria semina. Mkuu wa Wilaya Kilombero alifungua semina.

Tunapenda kuwashukuru wadau wetu Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Wilaya ya Kilombero, Benki ya NMB na CRDB kwa kushiriki na kusaidia semina.

# Kutoka Dawati Hans

by Hans Lemm

Kama mwaka mwingine unakaribia kuisha tunafurahi kusema KVTC inaendelea kukua. Hii siyo hatua ndogo katika mazingira yanayo ongezeka kuwa magumu ya kufanya kazi (na pia angalia kengele ya tahadhari kwenye Makala ifuatayo) na inazingatia jitihada na kujitoa kwa wafanyakazi wetu, wakandarasi na wabia wetu.

Robo ya mwisho 2018 ilikuwa ngumu na vua zilizo chelewa na hatimae tuliingia katika jitihada ya vita halisi ya kupambana na moto bahati mbaya ilipelekea kujeruhiwa kwa mmoja wa mfanyakazi wetu ambaye sasa hivi anapata nafuu katika hospitali Dar Es Salaam. Tunamtakia apone haraka na tunamatumaini atajumuika na familia yake nyumbani.

Soko limepitia msukosuko, kwa soko la ndani kupungua na baadhi ya bidhaa zetu kupata msukumo wa bei katika soko la nje.

Licha ya ugumu huu tunaendelea kuwekeza katika biashara na katika raslimali yetu ya msingi, watu wetu. Unaweza kusoma katika Makala yetu juu Mafunzo ya msimu wa Joto uzoefu ambao Geofrey amepitia. Vilevile tunafanya kazi na wawakilishi wa chama cha wafanyakazi juu ya mabadiliko ya masaa ya kazi ili kuruhusu muda zaidi wa mapumziko na kuboresha sehemu katika eneo la kiwanda ambayo itaanza kufanya kazi 2019.

Hii inaniacha niki watakia baraka za Krismas na furahia 2019 ambayo tutahakikisha tunaendelea kukushirikisha wewe juu ya maendeleo ya KVTC.



# Uvunaji haramu na Uvamizi

na Joseph John, Kennedy Haule & Hans Lemm



*Shamba la KVTC's Nakafulu Kwenye Google Earth likionyesha msitu uliopotea kuzungunguka eneo hilo la shamba.*

## Mlolongo wa kutisha

KVTC inasimamia eneo la hifadhi hekta 20,000 lenye msitu wa Miombo (16,00 hekta) na ardhi oevu na mbasa/mbuga (4000 hekta)

Mafanikio ya KVTC katika jitihada ya uhifadhi unaweza kuangalia kwa uwazi kabisa kwenye picha za Google Earth ambapo Msitu wa KVTC unaonekana kwa wazi na uharibifu wa misitu katika maeneo yanatuzunguka yamefikia kiwango cha kutisha na msitu wa KVTC ukiwa kwa uwiano bado upo mzima.

Changamoto ya mafanikio tunaona ongezeko la kiwango kikubwa cha uvunaji kote katika mashamba ya mitiki na vilevile katika msitu wa asili.

Licha ya uvunaji haramu tunaona ongezeko la kiwango cha uvamizi wa maeneo na wafugaji katika mashamba ya mitiki na kusababisha uharibifu mkubwa hususani kwenye mitiki midogo.

## Athari

KVTC inajisifia na ubora wa ardhi ya miombo tunayosimamia na tunaona athari chanya za mvua na ubora wa maji katika mashamba yetu. Uhifadhi wa misitu ya miombo unatengeneza mazingira maalumu ya hewa ambayo inafanya mitiki yetu kukua.

Bila msitu wa asili na bila mitiki michanga biashara yetu itaelekea kupungua ukuaji matokeo ni kupoteza ajira na fedha ikiwemo kodi.

## Ombi la Msaada wa Haraka

Kupitia Makala hii ya jarida tunapenda kuleta uharaka wa hali halisi kwa mamlaka na wadau wetu na kuomba msaada kuzuia mlolongo na kuhakikisha kwamba maeneo ya uhifadhi na mashamba ya mitiki ya KVTC ni salama kutokana na shughuli haramu.

KVTC imeajiri karibu askari wa mazingira 30 kwenye eneo hata hivyo kiwango kikubwa cha uvamizi bila ya msaada wa mamlaka (Wakala wa Misitu , Mamlaka ya usimamizi wa Wanyama pori, Malaka za Wilaya) hatuwezi kudhibiti hii hali.

### OSP PURCHASES 2018

Mwaka 2017 KVTC imeanza kununua magogo kutoka kwa wakulima wa nje na nusu ya pili ya 2018 tuliona ongezeko kubwa. Mwaka huu tumenunua karibu mita za ujazo 1,000m3 kutoka kwa wakulima wa nje kutengeneza mapato zaidi shillingi 250m kwa wakulima, wakandarasi,na mamlaka. Tunategemea kuongeza ujazo wetu 2019

### TUSIKILIZE

**Sikiliza Kipindi cha Mitiki Yetu**

Kwenye Radio Pambazuko 89.5FM

Kila Ijumaa 01.30 jioni na kila Jumamosi 01.30 asubuhi

### WASILIANA NASI

WASILIANA NASI AU TUANGALIE :
kvtc@kvtc-tz.com / http://kvtc-tz.com/

PO Box 655, Ifakara, TZ

PO Box 12452, Dar es Salaam, TZ